

Limejengwa katika Wagalatia 3:15-20.

A AGANO NA AHADI.

- ❖ Neno la kiyunani linalomaanisha “Agano” ni diathēkē. Lina maana mbili agano yaani mapatano na agano kwa maana ya toleo. Ni aina ya agano ambapo upande mmoja tu ndio hutoa ahadi kwa upande mwingiine. Kwa kawaida ahadi hutimizwa katika kipindi Fulani (kwa mfano, baada ya aliyeahidiwa kufa).
- ❖ Mungu huahidi nasi tunapokea. Ibrahimu aliipokea ahadi kwa imani. Daima Mungu hutimiza Ahadi zake (2 Wakorintho 1:20).

B AHADI NA SHERIA.

- ❖ Je; Sheria ilifuta agano la awali? Hapana. Je; utimizwaji wa ahadi[Kristo] ulifuta sheria? Hapana.
- ❖ Wokovu ni kwa imani katika ahadi, hivyo sheria haiwezi kutuokoa.

C KUSUDI LA SHERIA.

- ❖ Sheria ililetwa ili kutuonyesha hali yetu ya dhambi na kuyafumbua macho yetu yaone dhambi katika Maisha yetu (Warumi 7:13).
- ❖ Kauli “hata aje huyo mzao” inaweza kumaanisha kuwa sheria isingehitajika baada ya Kristo kuja. Hata hivyo, “hata” haimaanishi ni wakati gani hasa.
- ❖ Mafano, Yesu alisema: “Ila mlichio nacho kishikeni sana, hata nitakapokuja.” (Ufunuo 2:25) Hii haimaanishi kuwa hatutahitaji upendo au wema baada ya Yesu kuja...
- ❖ Sheria ilikuwa na kusudi zaidi ya kujaza nafasi kwa miaka 430 tangu ahadi ilipotolewa (Sinai) hadi kutimizwa (Kristo). Muda wa maisha ya sheria ni mrefu zaidi ya huo.
- ❖ Kwa mfano, Mungu alisema “Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu” (Mwanzo 26:5) Yusufu alijua kuwa uzizi ulikuwa ni dhambi kwa Mungu (Mwanzo 39:7-10). Waisraeli waliitunza Sabato ya Mungu hata kabla ya amri kutolewa (Kutoka 16:22-26).
- ❖ Sasa kwa nini mungu anatangaza amri Sinai kwa watu wa Israeli kupitia kwa Musa?
- ❖ Kwa sababu watu walikuwa wameisahau kwa kipindi walichokuwa utumwani misri.

D UKUU WA AGHADI.

- ❖ Sheria ile Mungu aliwapatia Israeli ni ya milele lakini haiwezi kuokoa.
- ❖ Kafara ya Yesu (Ahadi) ndiyo iliyoleta badiliko la kisa cha wokovu. Tangu wakati huo na kuendelea, kuna njia ya kuokolewa (hili lilitabiriwa na sheria sikukuu).
- ❖ Sheria ni muhimu, lakini haiwezikuchukua nafasi ya ahadi ya wokovu kwa neema na imani pekee. Ishukuriwe sheria, tunaweza kuelewa vyema jinsi ahadi ilivyo kitu bora.